

OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA Mtambo wa Kutengeneza Zege na Malori ya Kusafirishia Zege KUMB : ETJ-BB-PE-EI-GEN-SI-0001-00.

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Vifaa vya Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni na wataalamu wenye uzoefu kueleza nia zao kwa:

Mtambo wa Kutengeneza Zege na Malori ya kusafirishia zege Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni, eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

WIGO WA VIFAA / HUDUMA:

1. Mtambo wa kutengeneza Zege:

Kutafuta makampuni yenye mtambo wa kuzalisha takribani m3 3500 za zege kati ya Januari 2023 na Juni 2024.

2. Malori ya kusafirishia zege:

Kutafuta makampuni ambayo yanaweza kukodisha lori za kusafirishia / kubeba zege.

KIWANGO CHA MAHITAJI:

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Orodha ya uzoefu, rekodi za miradi inayoonyesha uzoefu katika kutengeneza na kusambaza zege.
- Wafanyakazi waliohitimu na kuthibitishwa kufanya kazi za kuthibiti Ubora/ Kuthibitisha Ubora (QA/QC)
- Mtambo wa kuzalisha Zege uliokaguliwa na kuthibitishwa Ubora (Hati ya Ubora ya Ulaya au Tanzania);
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha kusimamia kandarasi husika.
- Sera na Mpango Kazi wa Kampuni wa Usalama, Afya na Mazingira Eneo la Kazi.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, ni muhimu.
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi yarasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com; (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 5 September 2022, Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatahminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

Kumbuka: Kampuni zilizo hitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.